TANGAZO LA SERIKALI NA. 509 la tarehe 21/05/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

SHERIA NDOGO YA KUDHIBITI OMBAOMBA YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Afisa Mtendaji wa Kata" maana yake ni mtumishi yeyote wa umma aliyeajiriwa au kuteuliwa kutekeleza majukumu ya Mtendaji wa Kata iliyopo ndani ya eneo la Halmashauri;

"eneo la wazi" maana yake ni eneo lolote la ardhi lenye bustani au ambalo halijaendelezwa na lipo kwa ajili ya matumizi ya umma;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni;

"kituo cha hifadhi" maana yake ni kituo au mahali au jengo lolote ambalo limetengwa au linatumika katika kuwahifadhi ombaomba, wazee, watoto au watu wenye ulemavu kwa lengo la kuwapa mahitaji ya msingi;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi au anayefanya shughuli yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mtaa" maana yake ni eneo lolote lililopo ndani ya Halmashauri na inajumuisha maeneo yote ya barabara na hifadhi za barabara na njia ya waenda kwa miguu;

"ombaomba" maana yake ni mtu anayeishi kwa kutegemea kuomba chakula, fedha au kitu kingine kutoka kwa mtu mwingine kwenye mitaa na maeneo ya wazi yaliyoko ndani ya eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni au shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kudhibiti ombaomba

**4**.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kudhibiti ombaomba kwenye eneo lote la Halmashauri.

(2) Halmashauri inaweza kumteua wakala ambaye atatekeleza jukumu la kudhibiti ombaomba kwenye sehemu au eneo lote la Halmashauri kwa niaba ya Halmashauri.

(3) Kila Afisa Mtendaji wa Kata atakuwa na jukumu la kudhibiti ombaomba katika eneo lake la mamlaka.

Kutambua na kukamata

**5**.-(1) Mtu atakayekutwa mtaani au kwenye eneo la

ombaomba

wazi na Afisa Mwidhiniwa au wakala akiomba fedha au chakula kwa mtu mwingine atahesabika kuwa ni ombaomba na atakamatwa na kuchukuliwa taarifa zake muhimu ikiwemo:

(a) jina kamili;
(b) jinsi na umri; na
(c) kijiji, wilaya na mkoa anaotoka.

(2) Afisa Mwidhiniwa atampiga picha mtu yeyote atakayekamatwa kama ombaomba chini ya kanuni ndogo ya (1) na picha hiyo itatumika kwa matumizi ya Ofisi ili kurahisisha utambuzi iwapo mtu huyo atarudia kuwa ombaomba.

(3) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), ombaomba aliyekamatwa anaweza kufikishwa mahakamani kwa kutenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii.

Msaada kwa wenye mahitaji

**6**. Mtu, kikundi cha watu au taasisi yoyote inayohitaji kutoa msaada wa aina yoyote kwa watu wanaohitaji msaada itatakiwa kuwasilisha misaada hiyo kwenye kituo cha hifadhi, taasisi ya dini, kituo cha kulelea watoto yatima, wazee au watu wenye ulemavu na watu wengine wasiojiweza au Halmashauri.

Makosa

**7**.-(1) Mtu ambaye-

(a) anaomba na kupokea msaada wa fedha, chakula au kitu kingine chochote mitaani, kwenye maeneo ya wazi au mahali popote ambapo siyo kituo cha hifadhi;
(b) anatoa msaada wa fedha, chakula au kitu kingine chochote kwa ombaomba yeyote mtaani, kwenye maeneo ya wazi au mahali popote ambapo siyo kituo cha hifadhi;
(c) anamtembeza mtu yeyote kwa kutumia chombo chochote maalumu cha walemavu au kumtembeza kwa miguu au kwa njia nyingine yoyote kwa lengo la kuombaomba;

(d) anamsafirisha kutoka eneo moja hadi lingine mtu yeyote kwa lengo la kumtumia kuombaomba mitaani;

(e) anamtumikisha mtoto katika shughuli za kuombaomba kwenye magari, barabarania au mahali pengine popote;

(f) anashindwa kutoa taarifa au anatoa taarifa za uongo kuhusiana na ombaomba kwa lengo la kukwamisha upatikanaji wao ili wasiondolewe maeneo yasiyo rasmi; au

(g) anamzuia afisa yeyote au Wakala kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hii,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Adhabu ya jumla

**8.** Mtu anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii ambapo hakuna adhabu mahsusi iliyowekwa, anatenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi mitatu au vyote.

Ufifilishaji wa makosa

**9**.-(1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kinyume cha Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu hamsini iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali.

(2) Pamoja na mamlaka ya Mkurugenzi kufifilisha kosa chini ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kumrejesha mtu yeyote aliyekamatwa ndani ya maeneo ya Halmashauri akiwa ombaomba kwenye mkoa anaotoka na kumkabidhi katika Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa husika.

# JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 10(1))*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya nanuni ya ………ya Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni, niko tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU**

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………
Jina……………………………….. Saini………………………

**MBELE YANGU:**
Jina: …………………………………..………………………
Saini……………………….……………………….………
Wadhifa: ……………………………………………………….
Tarehe………………………………………………………….

*Tangazo La Serikali Na. 509 (Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imegongwa kwenye sheria ndogo hii kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni uliofanyika tarehe 24 mwezi 08 Mwaka 2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya ;

HANIFA SULEIMAN HAMZA
*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri*
*ya Manispaa ya Kinondoni*

SONGORO KHAMISI MNYONGE
*Mstahiki Meya wa Halmashauri*
*ya Manispaa ya Kinondoni*

NAKUBALI

L.S

Dodoma
10 Disemba, 2023

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais*
*(Tawala za mikoa na serikali za mitaa)*